TANGAZO LA SERIKALI NA. la tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA KILIMAHEWA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Kilimahewa ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala.

*Tangazo la serikali na. (linaendelea)*

________

JEDWALI

________

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia katika barabara ya Mtama - Newala kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba K1 yenye majira - nukta 536399MS, 8822585KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $70^0$ 00'58'' kwa umbali wa kilomita 0.572 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba K2 yenye majira - nukta 535861MS, 8822389KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $19^0$ 13'05'' kwa umbali wa kilomita 0.239 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba K3 yenye majira - nukta 535783MS, 8822616KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa $04^0$ 53'44'' kwa umbali wa kilomita 0.705 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba K4 yenye majira - nukta 535722MS, 8823319KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini- Mashariki katika uelekeo wa $78^0$ 01'07'' kwa umbali wa kilomita 0.108 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba K5 yenye majira - nukta 535828MS, 8823341KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $71^0$ 37'14'' kwa umbali wa kilomita 0.343 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba K6 yenye majira - nukta 536153MS, 8823233KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa kufuata barabara ya Mtama -Newala hadi ulipoanzia."

Dodoma,
………., 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*